

# \*Ufugaji kuku sasa kunufaisha wananchi

**Na Mwandishi Wetu,  
Zanzibar**

**K**ATIKA kuhakikisha utaratibu wa 'SAGCOT model' unaotumika na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanja za Juu Kusini mwa Tanzania unaenea nchini na kuleta mafanikio makubwa katika sekta za kilimo na mifugo, Zanzibar imeanza kunufaika na mafunzo ya ufugaji kuku.

SAGCOT kwa kushiriki-

ana na Kampuni ya Silverlands inayozalisha vifaranga na kuzalisha chakula cha kuku wameanza kutoa mafunzo ya ufugaji wa kisasa wa kuku wenye tija na kilimo na kuhamasisha kilimo na ufugaji kibiareshara.

Akizungumza mjini Unguja katika mkutano na wadau wa kilimo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga aliwataka wananchi wa Zanzibar kuachana na kilimo cha mazoea na badala yake wajikite kwenye kilimo cha

kisayansi ambacho kitatoa matokeo chanya.

"Zanzibar haina sababu ya kuagiza bidhaa za vyakula nje ikiwa maeneo ya kufanya ufugaji na kilimo yapo, kikubwa ni utayari wa kupokea elimu ya ufugaji na kilimo cha kisasa," alisema.

Alisema miaka mingi Zanzibar imekuwa ikiingia gharama kubwa kwa kuagiza bidhaa nyingi nje hivyo kupunguza hamasa kubwa ya uzalishaji mazao ikiwemo nyama ya kuku.

"Soko la kuku ni kubwa Zanzibar wananchi wakitumia fursa hii kufanya ufugaji wa kisasa wa kuku, maisha yatabadilika kiuchumi na kuchangia maendeleo ya taifa," alisema.

Kirenga aliomba wananchi waliopewa mafunzo ya ufugaji wa kuku kuzingatia mafunzo hayo ili wafanye ufugaji wa kisasa utakaowaletea tija katika uzalishaji na kuongeza vipato vyao.

"Silverlands Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa SAGCOT katika ufugaji

na uzalishaji wa chakula cha mifugo, tutashirikiana nao kutoa elimu ya ufugaji bora wa kuku," alisema.

Alisema katika ubia na Silverlands Tanzania, kazi kubwa ya uzalishaji chakula cha mifugo, elimu ya ufugaji bora wa kuku imefanyika Iringa, Njombe na Mbeya na mafanikio kwa wafugaji katika kuongeza uzalishaji na kipato.

"Tunataka na Zanzibar iachane na kuagiza kuku nje. Tutatoa elimu ya ufugaji bora wa kuku ili kuongeza

uzalishaji na kutoa fursa kwa watu wengi wajajiri kwa ufugaji," alisema Kirenga.

Meneja Masoko wa Silverlands Tanzania, Ahmed Abdul Rahman alisema wamejipanga kutoa elimu bora ya ufugaji wa kisasa kuku ili kutanua wigo wa uzalishaji nyama nchini.

"Tutahakikisha mahita muhimu yanapatikana kw wafugaji ikiwemo vifaran bora, chakula cha mifugo na dawa za kukinga kuku alisema.

## Ujenzi stendi mpya Dar waanza Mbezi

**Na Oscar Job**

**U**JENZI wa stendi ya mpya na kisasa ya mabasi umeanza katika eneo la Mbezi Luis Jijini Dar es Salaam baada ya kukamilika kwa mchakato ukiwemo

